



Pia, bidhaa zikisha tengenezwa bado hutegemea usahihi wa vipimo wakati wa kufungashwa katika ujazo, urefu au uzito mbalimbali tayari kwa kusambazwa katika masoko.

Afya

Sekta ya afya hutegemea vipimo katika kuyafikia malengo yake kiutendaji.

Katika hospitali, zahanati na vituo vya afya, madaktari na wauguzi hutegemea vipimo mbalimbali vya wagonjwa kama uzito, msukumo wa damu (*Blood Pressure*), joto, n.k. Ili kuweza kuamua tiba sahihi kwa wagonjwa.

Mfano: Bila kutumia vipimo sahihi daktari anaweza kumweleza mgongwa kutumia kiasi cha dawa ambacho kinaweza kuhatarisha maisha yake.

Mfano: Bila kutumia vipimo sahihi ni vigumu kufahamu maendeleo ya mama mjamzito na hivyo kushindwa kumpa huduma anayostahili katika kipindi chote cha ujauzito.

Usalama

Vyombo mbalimbali vya usalama vinavyotumiwa na maaskari barabarani ni lazima viwe sahihi kwa ajili ya kutoa matokea sahihi kwa watumiaji. Mfano, *traffic speed radar* lazima vipimo vya ke viwe sahihi kwa ajili ya kutolea maamuzi sahihi.

Kwa Mawasiliano zaidi;

Afisa Mtendaji Mkuu

Wakala wa Vipimo, Mtaa wa Uhuru,
Orofa ya saba, Jengo la NSSF – Mafao,
S.L.P 313, Dar es salaam,
Simu: +255 (022) 2928156, Namba ya
Malalamiko: +255 (0) 653 383 953,
Barua pepe: info@wma.go.tz,
Tovuti: www.wma.go.tz



Kuhusu
**WAKALA
WA VIPIMO
(WMA)**

Utangulizi

Kama ilivyoanishwa katika Sera ya Taifa ya Biashara, Wakala wa Vipimo ni Taasisi mojawapo ya Umma inayowezesha utekelezaji wa malengo mbalimbali ya Taifa katika uchumi hasa katika biashara. Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa liitwalo *International Organisation for Legal Metrology (OIML)*, haina budi kusimamia usahihii wa vipimo halali vinavyotumika katika biashara kwa maslahi ya wananchi wake na kwa ajili ya uwiano mzuri wa Kimataifa. Umuhimu wa vipimo uko dhahiri katika maeneo ya kumlinda mlaji, usafiri na Usafirishaji, taarifa za uchumi, kilimo, viwanda, afya, usalama, mazingira pamoja na uhakiki mali ulio sahihi.



Maafisa Vipimo wakifanya uhakiki wa mita za maji

MAJUKUMU YA WAKALA WA VIPIMO TANZANIA

Kumlinda mlaji

Mlaji kupata bidhaa sawa na thamani ya fedha zake

- Kuondoa utata katika biashara baina ya muuzaji na mnunuzi
- Kuleta haki na usawa katika biashara kwa kuondoa matumizi ya vipimo visivyo sahihi.



Usafiri na Usafirishaji

Vyombo vya usafiri vitumikavyo kubeba bidhaa/mizigo au abiria vinatakiwa kuzingatia vipimo kwa kubeba mizigo kulingana na uwezo wake, na hivyo kuepuka ajali na uharibifu wa miundombinu kama barabara na reli.



Magari yakipita kwenye Mizani kuhakiki uzito wa mizigo iliyobebwa

Taarifa za uchumi

Taarifa zinazotolewa na sekta mbalimbali kuhusu uzalishaji, biashara na uchumi hutegemea vipimo. Kwa mfano; Taarifa kuhusu mauzo ya bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi hutegemea vipimo, kama vile tani milioni ishirini za Pamba, lita milioni tano za maziwa, mita milioni hamsini za vitambaa vya nguo, n.k. hivyo, matumizi ya vipimo sahihi ni muhimu katika upatikanaji wa takwimu sahihi.

Kilimo

Uchumi wa Tanzania hutegemea kilimo kwa karibia asilimia hamsini, na karibu asilimia themanini ya wananchi wake hutegemea kilimo au shughuli zenyen uhusiano na kilimo. Serikali imeipa sekta ya kilimo kipaumbele kwa kuhakikisha kuwa pembejeo na zana za kilimo zinapatikana kwa bei nafuu ili mkulima aongeze tija na kupata thamani halisi ya jasho lake kwa kuwa na vipimo sahihi vya malighafi mfano Pembejeo, n.k na mwisho auze mazao yake kwa vipimo sahihi.

Wakulima wakiuza mazao yao kwa kutumia vipimo sahihi ni lazima uzalishaji utaongezeka Viwanda vingi vitajengwa kwa kuwa malighafi zinazotumika viwandani zitakuwa nyngi na kupelekea kukua kwa uchumi wa Viwanda kama ilivyo adhima ya Serikali ya awamu ya tano kukuza uchumi wa Viwanda.

Viwanda

Bidhaa zinazotengenezwa viwandani hutegemea vipimo ambavyo hutumika kupima malighafi na mahitaji mengine.